HALMASHAURI YA MANISPAA YA DODOMA

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASIKINI (PSSN) TASAF AWAMU YA TATU YA MWAKA 2016/2017

KWA WAJUMBE WA KAMATI YA MAANDALIZI YA MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI AWAMU YA PILI.

1. UTANGULIZI

Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma ni mojawapo ya Halmashauri nane za Mkoa wa Dodoma zinazotekeleza Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini. Manispaa ya Dodoma ina Mitaa 170 na Vijiji 18. Mpango huu ulizinduliwa katika Manispaa hii mwezi Aprili 2014. Aidha wakati wa uanzishwaji wa Mradi wa TASAF III Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma ilikuwa na Vijiji vingi hivyo Mradi wa TASAF III uko katika Vijiji 25 na Mitaa 48 inayotambulika na Mradi.

2. MADHUMUNI

Madhumuni ya Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini ni kuwezesha kaya zinazoishi katika hali duni kuongeza kipato, fursa na uwezo wa kugharamia mahitaji muhimu katika kaya zao.

3. UTEKELEZAJI WA MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI

3.1 MCHAKATO WA UTAMBUZI WA KAYA MASKINI

Mchakato wa utambuzi wa kaya maskini ulifanyika kwa kuanza na semina elekezi kwa viongozi na baadhi ya watumishi wa Manispaa ya Dodoma ambao walielimishwa kuhusu taratibu za utambuzi wa kaya maskini. Baada ya semina hiyo watumishi wa idara mbalimbali kama vile maendeleo ya jamii, elimu, kilimo, mifugo, afya na mipango walipangiwa mitaa/vijiji vya kusimamia zoezi la utambuzi wa kaya maskini ambao ulikuwa unafanywa na wakusanya taarifa waliochaguliwa katika mtaa/kijiji husika.

Hatua zifuatazo zilitumika kuwapata walengwa wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini:

- Kufanya mikutano na viongozi wa Mtaa/Kijiji kwa ajili ya kuwaelimisha kuhusu Mpango, vigezo vya umaskini na hatua za kufuatwa ili kuwapata walengwa.

- Mkutano Mkuu wa Mtaa/Kijiji ulifuata baada ya kikao cha viongozi wa Mtaa/Kijiji. Wananchi walielezwa malengo, madhumuni na vigezo vya umaskini na walishiriki katika kuweka vigezo hivyo.

- Wakusanya taarifa walichaguliwa katika Mkutano Mkuu wa Mtaa/Kijiji ambao walipewa semina ya siku moja kuhusu vigezo vya umaskini na hatua za kufuata katika kuandaa orodha ya awali ya kaya maskini katika Kijiji/Mtaa husika. Orodha hiyo ilihakikiwa na viongozi wa Mtaa/Kijiji baadae kuthibitishwa na Mkutano Maalumu wa Mtaa/Kijiji.

- Walengwa waliopitishwa na Mkutano Maalumu wa Mtaa/Kijiji walijaziwa madodoso ambayo yaliwasilishwa Manispaa na baadae TASAF Makao Makuu.

3.2 IDADI YA KAYA MASKINI:

Baada ya mchakato wa utambuzi wa kaya maskini, jumla ya Kaya 12,272 zilitambuliwa ambapo kati ya hizo Kaya 8,100 ziliioorodheshwa na kuthibitishwa na Mkutano Mkuu Maalum wa Kijiji/Mtaa husika. Wakati wa utekelezaji wa Mpango ilibainika uwepo wa Kaya ambazo hazistahili kuwa katika Mpango na utaratibu wa kuziondoa ukafanyika na wengine hupunguzwa kutokana na kufariki au kuhama hadi kufikia sasa jumla ya kaya 6,468 zimebaki kwenye Mpango kati ya 8,100.

3.3 UHAWILISHAJI FEDHA:

Utaratibu wa uhawilishaji fedha unafanywa na wananchi wenyewe kupitia Kamati ya Usimamizi ya Mpango (CMC) yenye wajumbe 14 chini ya usimamizi wa viongozi wa Kijiji/Mtaa na mtaalam ngazi ya Wilaya au Kata. Wajumbe hao hugawanywa katika makundi mawili ya wajumbe 7 na kila Mjumbe ana kazi maalumu kama vile kufuata fedha benki wakati wa malipo, kufuatilia fomu za Masharti ya Elimu na Afya na kutoa elimu kwa walengwa juu ya matumizi ya fedha.

Kamati hizi zilichaguliwa na wananchi wenyewe kwenye Mkutano Maalum wa Kijiji/Mtaa uliofanyika wakati wa kuandikisha Kaya Maskini.

Jumla ya Tsh **1,321,256,000.00** zimehawilishwa kwa walengwa kwa awamu saba kama ilivyoainishwa kwenye jedwali hapa chini.

NA	KIPINDI CHA MALIPO	KIASI KILICHOPO KELEWA	KIASI KILICHOLIPWA KWA WALENGWA	KIASI KILICHORUDI SHWA TASAF MAKAO MAKUU	FEDHA ZA USIMAMIZI HALMASHAURI	FEDHA ZA MTAA/KIJIJI
1	Julai-Aug 2016	278,163,000.00	245,572,000.00	1,684,000.00	23,882,681.82	4,214,590.91
2	Sept-Oct 2016	275,553,000.00	242,468,000.00	2,468,000.00	23,658,590.91	4,175,045.45
3	Nov-Dis 2016	244,796,000.00	243,328,000.00	1,468,000.00	23,645,068.18	4,172,656.00
4	Jan-Feb 2017	214,137,000.00	198,308,000.00	1,036,000.00	18,385,500.00	3,244,500.00
5	Mach-Apr 2017	220,738,500.00	194,692,000.00	1,520,000.00	18,952,295.45	3,344,522.73
6	Mei-Jun 2017	222,210,795.00	196,888,000.00	1,112,000.00	15,815,000.00	7,300,000.00
7	Julai-Aug 2017	216,866,795.00	-	-	15,815,795.00	7,300,000.00
	JUMLA	**1,672,465,090.00**	**1,321,256,000.00**	**9,288,000.00**	**140,154,931.40**	**33,751,315.09**

3.4 MIRADI YA AJIRA ZA MUDA:

Miradi ya Ajira za Muda ina lengo la kumuongezea kipato mlengwa wakati wa kipindi cha *Ari* na kupata ujuzi kwa kufanya kazi katika Miradi, Miradi hiyo iliibuliwa na walengwa wenyewe na pia inatumia teknolojia ya nguvu kazi. Kwa Maanispa ya Dodoma Miradi hiyo ilitekelezwa mwezi wa Septemba,2016 hadi Disemba, 2016. Jumla ya Miradi 80 iliibuwa katika Mitaa/Vijiji 73 kwa kipindi hicho na miradi iliyotekelezwa ilikuwa 75 kwa sababu baadhi ya Mitaa/Vijiji viibua mradi zaidi ya mmoja. Miradi hiyo ni uchimbaji/ukarabati wa mabwawa, makinga maji, usafi wa mazingira na upandaji wa vitalu vya miti. Baada ya kufanya tathmini ya Miradi iliyotekelezwa ilionekana miradi ya usafi wa

mazingira haikuwa na thaman ya pesa na haiwapi walengwa ujuzi wowote utakao wezesha upatikanaji wa chakula hivyo miradi hiyo haitafanyika tena. Kwa mwaka 2017 miradi iliyoibuliwa ni 60 na itatekelezwa Mwezi Septemba 2017 hadi Disemba 2017.

Jumla ya Tsh**872,657,991.00** zililipwa kwa walengwa kama ujira kwa kufanya kazi katika kipindi cha miezi minne kama ilivyoainishwa kwenye jedwali hapa chini:

NA	KIPINDI CHA MALIPO	KIASI KILICHOPO KELEWA	KIASI KILICHOLIPWA KWA WALENGWA	KIASI KILICHORUDISHWA TASAF MAKAO MAKUU	FEDHA YA USIMAMIZI HALMASHAURI	FEDHA YA MTAA/KIJIJI
1	Sept 2016	215,454,291.00	210,690,991.00	4,763,300.00	-	-
2	Oct 2016	231,702,000.00	230,526,900.00	1,175,100.00	-	-
3	Nov 2016	218,035,400.00	431,440,100.00	1,272,000.00	51,719,260.41	8,970,013.21
4	Dis 2016	214,676,700.00				
	JUMLA	**2,842,186,991.00**	**872,657,991.00**	**7,210,400.00**	**51,719,260.41**	**8,970,013.21**

3.5 MRADI WA MIUNDOMBINU:

Ujenzi wa nyumba ya Mwalimu Kijiji cha Gawaye, ujenzi wa nyumba hiyo umegharimu kiasi cha Tsh **62,198,920.00**, ambapo Tsh **58,034,520.00** zilitumika kwenye ujenzi wa nyumba na Tsh **4,164,400.00** zilikuwa kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji. Nyumba hiyo imekamilika na imeombewa cheti cha ukamilifu.

3.6 AINA YA RUZUKU ZINAZOTOLEWA

Ruzuku ya Msingi

Ruzuku hii inatolewa kwa Kaya zilizomo kwenye Mpango kiasi cha shilingi 10,000/= kwa mwezi, endapo Kaya ina watoto wa kuhudhuria shule au kliniki itaongezwa shilingi 4,000/=

Ruzuku ya Masharti

Ruzuku hii inatolewa kwa watoto wanaohudhuria shule na kliniki.

- Mtoto chini ya miaka 5 atalipa shilingi 4,000/= kwa kuhudhuria kituo cha Afya kila mwezi.

- Mtoto/ watoto wanaosoma shule ya msingi watalipwa shilingi 2,000/= kwa kila mtoto kwa watoto wasiozidi 4 katika Kaya kwa mwezi.

- Mtoto/watoto wanaosoma sekondari watalipwa shilingi 4,000/= kwa kila mtoto kwa watoto wasiozidi 3 katika Kaya kwa mwezi.

- Mtoto/watoto wanaosoma sekondari kidato cha tano na sita watalipwa shilingi 6,000/= kwa kila mtoto kwa watoto 2 katika Kaya kwa mwezi.

3.7 MASHARTI YA MPANGO

- Mtoto wa umri chini ya miaka 5 kuhudhuria kliniki kila mwezi.

- Mtoto wa shule mahudhurio yake yasiwe chini ya asilimia 80.

3.8 CHANGAMOTO ZA MPANGO

- Mitaa 112 haiko kwenye Mpango na Vijiji 3 haviko kwenye Mpango.

- Baadhi ya kaya kutojitokeza wakati wa malipo

3.9 MAFANIKIO YA MPANGO

Baada ya awamu saba za uhawilishaji fedha na awamu nne za malipo ya ujira kwa walengwa mafanikio chanya yameonekana kama ifuatavyo:

- Mahudhurio ya watoto shuleni yameongezeka toka watoto 2,954 hadi kufikia watoto 6,429.

- Mahudhurio ya watoto kwenye vituo vya Afya yameongezeka toka watoto 1,985 hadi kufikia watoto 2,261 kwa ajili ya kupima maendeleo ya ukuaji wao na kuboresha lishe kwa watoto.

- Baadhi ya Kaya zimeanzisha biashara ndogondogo kwa ajili ya kujiongezea kipato katika Kaya.

- Baadhi ya walengwa wamejiunga na mfuko wa Bima ya Afya (CHF) Iliyoboreshwa.

4. HITIMISHO:

Tunashukuru Serikali kupitia **TASAF** kwa kuwa na Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini hususani katika Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma, kwani imesaidia kupunguza umaskini na kuwapatia walengwa ujuzi kupitia miradi ya Ajira za Muda. Tutaendelea kushirikiana na kuhakikisha malengo ya Mpango wa kunusuru Kaya Maskini yanafikiwa.

Godwin E. Kunambi
MKURUGENZI WA MANISPAA,
DODOMA.

.